## Mstahiki Mheshima Raila Amolo Odinga

# Kauli ya Maono kwa Nafasi ya Mwenyekiti wa Tume ya Muungano wa Afrika (AUC)

Iwapo karne hii itakuwa karne ya Afrika, na tutafurahia enzi mpya yenye ustawi na amani, basi ni lazima tutumie kikamilifu rasilimali watu na maliasili tele tuliyonayo, huku tukijumuisha nguvu za vijana wetu pamoja na maono na hekima ya viongozi wetu. Katika wakati huu muhimu, ambapo fursa zetu za mafanikio zinatishiwa na changamoto nyingi za kilimwengu, tunahitaji Tume ya Muungano wa Afrika (AUC) yenye uwezo wa kufanikisha vipaumbele vya Waafrika – kwa kuchochea maendeleo na kuipa bara la Afrika ushawishi unaostahili ulimwenguni.

Kama aliyeamini falsafa ya uafrika maishani mwangu wote, ambaye pia ametumikia nchi yangu barani Afrika na bara la Afrika ulimwenguni kote, kiongozi ambaye amefaulu katika nafasi zote ambazo nimetumikia – mashinani, kitaifa na kimataifa, ninaamini kwamba ninafaa zaidi kutumikia bara langu na Nchi Wanachama wa Muungano wa Afrika katika nafasi hii muhumu kama mwenyekiti wa Tume ya Muungano wa Afrika.

Ili kuafikia haya, nimeweka mipangilio na mikakati ifuatayo kukabiliana na changamoto zinazokumba bara la Afrika.

## 1. Mageuzi ya Kiuchumi

Ukuaji wa kiuchumi endelevu na wenye usawa ni msingi wa maendeleo yetu. Nitasukuma miradi inayobuni mazingira mazuri ya biashara kustawi na kuvutia uwekezaji ili kukuza uvumbuzi na ujasiriamali. Nitaendeleza sera zinazobuni nafasi za ajira, kupunguza umaskini na kuboresha maisha. Nina azma ya kuchochea maendeleo ya viwanda, kupanua sekta ya uzalishaji, kuimarisha uvumbuzi, uwekezaji katika elimu, afya, nishati nafuu na maendeleo ya ujuzi.

## 2. Kuimarisha Biashara ya ndani kwa ndani barani Afrika

Eneo Huru la Biashara la Afrika (AfCFTA) ni fursa nzuri ya kuanzisha soko la pamoja na kuongeza biashara ya ndani ya Afrika. Kwa sasa, biashara ya ndani ya Afrika ni ndogo kuliko mabara mengine, jambo linalozuia uhuru wetu wa kiuchumi na utegemezi. Nitapigania anga za wazi, usawa wa sera za visa, na maendeleo ya miundombinu kufanikisha mwingiliano wa bidhaa na watu kote Afrika. Kuvuka vikwazo hivi kutachochea ukuaji wa kiuchumi na kuweka Afrika kama mdau na kiongozi wa kiuchumi kimataifa.

## 3. Uhuru wa Kifedha

Afrika lazima itumie rasilimali za ndani ili kupunguza utegemezi na kutegemea ufadhili kutoka nje. Nitasukuma Mataifa Wanachama na kushirikisha sekta binafsi kufadhili vipaumbele vya AU, kuhakikisha maendeleo endelevu na utekelezaji wa malengo ya bara. Nitapigania marekebisho ya muundo wa kifedha ulimwenguni kuzingatia mahitaji ya Afrika, kuhakikisha usawa katika maamuzi ya kiuchumi ya ulimwengu.

## 4. Usawa wa Jinisia

Hakuna kikundi katika jamii ambacho kinapitia mazingira magumu kutokana na changamoto zinazokumba bara la Afrika kama wanawake na wasichana. W[illegible]

waathiriwa wa ukatili wa kijinsia na katika nyanja zote ikiwemo elimu, afya, chakula, uhuru wa kifedha na ajira. Malengo ya ajenda ya 2063 ya Afrika hayawezi kutimizwa iwapo kutengwa na kubaguliwa kwa wanawake na wasichana hautakomeshwa. Kama Mwenyekiti wa Tume ya Muungano wa Afrika, nitaipa kupaumbele nafasi, heshima na usalama wa wanawake na wasichana kote barani Afrika.

5. **Ubadilishaji wa Kilimo**

Afrika inahitaji kubadilisha mfumo wake wa kilimo ili kukuza mazoea ya kilimo yenye ufanisi, usiyo na ubaguzi na unaohimili mabadiliko. Nitakuza uzalishaji endelevu wa chakula na biashara ya kilimo ili kuimarisha usalama wa chakula, kuchochea uumbaji wa ajira, na kuboresha maisha ya vijijini. Isitoshe, nitahakikisha kwamba mifumo ya chakula barani Afrika ni huru na iliyokingwa dhidi ya sera kandamizi. Nitajitahidi kuhamasisha upatikanaji wa masoko ndani ya bara na kuongeza thamani katika sekta zetu za kilimo na uvuvi. Juhudi hizi za pamoja zitahakikisha maendeleo endelevu na kukabiliana na njaa katika bara letu.

6. **Hatua za Mabadiliko ya Tabianchi**

Mwanzo, azma yangu ni kuhakikisha kwamba Waafrika hawaadhibiwi kwa tatizo ambalo hawajasababisha. Kwa hiyo, umakini wangu ni kuhamasisha usaidizi unaostahili kwa kustahimili athari za mabadiliko ya tabianchi, kuweka mifumo bora ya tahadhari za mapema na majibu kwa mishtuko ya tabianchi. Zaidi ya hayo, nitakuza uwekezaji na fedha zinazofaa kwa tabianchi, kutumia rasilimali za nishati mbadala, na kuingiza mikakati ya kisasa ya tabianchi katika mipango yetu ya kiuchumi, kwa ajili ya kuhakikisha mustakabali endelevu kwa Afrika. Kwa umuhimu, nitazidisha sauti ya Afrika katika mikutano ya kimataifa kuhusu mabadiliko ya tabianchi, hatua dhidi ya tabianchi na haki kwa athari za tabianchi.

7. **Ushirikiano Barani**

Kuimarisha ushirikiano wa kikanda ni muhimu kwa kukuza biashara, maendeleo ya miundombinu, na ukuaji wa kiuchumi. Nitaiunga mkono Jumuiya za Kiuchumi za Kikanda na kusukuma utekelezaji wa miradi ya kuimarisha umoja na ustawi wa bara.

8. **Amani na Usalama**

Amani na usalama ni nguzo muhimu kwa maendeleo. Kwa hivyo, nitaweka kipaumbele katika utatuzi wa mizozo, kushirikiana na viongozi wa Afrika barani kote kupambana na sababu kuu za misukosuko, na kuimarisha taasisi zenye ufanisi ili kuunda mazingira yanayofaa kwa maendeleo na ustawi wa Afrika.